

JARIDA KUHUSU |UTALII | UHIFADHI NA MASUALA MBALIMBALI

# TZ&BEYOND

Multisectoral magazine

NOVEMBER-DECEMBER, 2022 | ISSUE NO 003

## SGR KICHOCHEO CHA UCHUMI TANZANIA

**39** **MRADI** HUU UTAPUNGUZA GHARAMA ZA USAFIRISHAJI

TSHS.25,000 KSHS.1,300 USHS 40,000

ISSN 2799-225X | LESENI 00000021
www.tz&beyond.co.tz







# BODI YA WAHARIRI

AFISA MTENDAJI MKUU
Emmanuel J. Kakuyu
Cell: 0622411148
ekakuyu@gmail.com

MHARIRI MTENDAJI
Jimmy C. Kiango
Cell: 0787 180 065
jimmy.kiango@tz&beyond.co.tz

MSANIFU KURASA
Felix Jimmy
Cell: 0763 520 319
felix.aloyce@tz&beyond.co.tz

MWANDISHI
Hassan Daud
Cell: 0692 695 889

MWENYEKITI/MLEZI
Dk. Thomas Kashililah
[fclpp, cipm,ChE, AFA]
Cell: 0754 997 645
namkonda@gmail.com

**TZ&BEYOND**
Mbezi Beach Park Building;
Off Bagamoyo Road
P.O. Box 79010, Postcode: 14121
Phone: +255 655 06 38 39
Dar Es Salaam , Tanzania

**MAUZO/MATANGAZO**
Sales Team,TZ&BEYOND
Cell: 0655063839
email: tz1andbeyond@gmail.com





www.tz&beyond.co.tz



39 MRADI HUU UTAPUNGUZA GHARAMA ZA USAFIRISHAJI



34 TRC na maendeleo ya SGR



24 Maana ya SGr



21 Rais Samia auongezea kasi ujenzi wa SGR



07 SGR kwa maendeleo ya tanzania



45 Tanzania nchi ya kwanza Afrika mashariki na Kati kuwa na treni inayotumia nishati ya umeme



30 Gharama za mradi



24 Waziri Mkuu: Mradi utakamilika kwa wakati







34 SGR kwa maslahi ya Tanzania



## JICHO LA TZ&BEYOND



AFISA MTENDAJI MKUU: EMMANUEL J. KAKUYU
JARIDA: TZ&BEYOND
COVER STORY: SGR KWA MAENDELEO YA TAIFA

# SGR KICHOCHEO CHA UCHUMI TANZANIA

KAZI ya kuifungua nchi kitaifa na kimataifa inaendelea. Serikali ya Rais Samia Suluhu Hassan inatekeleza kile ilichoahidi.

Miradi mikubwa na midogo inaendelea kutekelezwa kwa kasi. Hali hiyo inabeba nia njema ya Rais Samia mwenyewe ya kuendeleza miradi yote ya kimkakati.

Miongoni mwa miradi hiyo ni mradi wa ujenzi wa Reli ya kisasa (SGR), ulioanza rasmi mwanzoni mwa mwaka 2017, wakati wa utawala wa serikali ya awamu ya Tano.

Ujenzi huo wa Reli hiyo wenye faida lukuki kwa nchi na wananchi wake unafanyika sanjari na mfumo wa reli ya zamani inayotumia geji ya mita moja.

Ujenzi Reli ya SGR yenye upana wa milimita 1,435 unatazamwa kama mradi unaolenga kuwa na manufaa makubwa , ambapo utaiunganisha Tanzania na nchi jirani

Nchi zitakazoungana na Tanzania kupitia Reli hiyo ni Rwanda, Uganda, Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo.

Hakuna shaka yoyote reli hiyo itapunguza gharama za usafirishaji wa bidhaa kati ya bandari ya Dar es Salaam na Kigali, nchini Rwanda, Bujumbura -Burundi, na hatimaye Goma - Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo .

Aidha uwepo wa reli hiyo ambao hadi kukamilika kwake katika vipande vitano utakuwa umegharimu shilingi trilioni 23.3, utasaidia kuamsha uchumi wa mikoa ya Kanda ya ziwa pamoja na kupunguza sana gharama za usafiri na usafirishaji wa mizigo.

Ni wazi bandari zilizopo kwenye ukanda huo zitasafirisha bidhaa kati ya Mwanza na Port Bell karibu na jiji la Kampala, mji mkuu wa Uganda.

Jicho la TZ&BEYOND linaamini kupungua kwa gharama za usafiri na usafirishaji kutapunguza gharama za uzalishaji bidhaa za viwandani na kilimo hali itakayosaidia kupunguza mfumuko wa bei za bidhaa.

Pamoja na hilo, lakini pia mradi huo utaiongezea uwezo reli ya kati, utapunguza gharama na muda wa usafirishaji, utalinda barabara, utasafirisha mizigo na abiria wengi kwa pamoja na kuepuka msongamano wa malori na mabasi barabarani.

Kuongezeka kwa mzunguko wa fedha na kuwepo kwa fursa za ajira. Kuboreshwa kwa huduma za kijamii kwa wakazi wa maeneo ya mradi, kuboreshwa kwa kilimo kupitia upatikanaji wa urahisi wa pembejeo za kilimo

Kwa sasa utekelezaji wa mradi huu unaendelea na Januari 18,2023,Makamu wa Rais Dkt. Philip Mpango akiwa mkoani Shinyanga, alizindua rasmi ujenzi wa kipande cha nne kinachoanzia Isaka-Shinyanga-Mwanza (km 220).

Jicho la TZ& BEYOND limeshuhudia kukamilika kwa kiasi kikubwa kwa vipande vitatu vya Dar es Salaam-Morogoro (km 300), Morogoro-Makutopora (km 426),Makutopora-Isaka (km 435), ambavyo vimebeba zaidi ya stesheni kubwa na ndogo 15.

Kampuni ya Yapi Merkezi kutoka Uturuki ndio imefanikiwa kujenga kipande cha kwanza, cha pili na cha tatu, huku ikishirikiana na kampuni ya Mota-Engil ya Ureno katika ujenzi wa kipande cha kwanza.

Kipande cha nne kinajengwa kwa pamoja na kampuni za China Civil Engineering Corporation CECC na China Railways Construction Corporation CRCC.

Aidha pamoja na mafanikio yaliyofikiwa, lakini mradi huo ulikabiliwa na changamoto kadhaa zilizosababisha kuchelewa kukamilika kwake kwa wakati.

Jicho la TZ&BEYOND limeenda mbali zaidi na kugundua changamoto kubwa iliyokuwapo hadi kufikia hatua ya kusogeza mbele muda wa kumaliza mradi ni uhaba wa fedha za ndani za kugharamia awamu zote za mradi huo.

Hata hivyo changamoto hii imeshapatiwa ufumbuzi na Serikali ya awamu ya Sita baada ya kupata mkopo wenye masharti nafuu.

Aidha uwepo wa mvua kubwa katika eneo la mradi hasa wakati wa ujenzi wa kipande cha kwanza na cha pili kuliathiri kasi ya mradi na muda wa kukamilisha awamu hiyo.

Jicho la TZ&BEYOND linaamini mradi huu wa SGR ambao umechambuliwa kwa kina kwenye jarida hili, una faida nyingi na utakuwa kichocheo cha ukuaji wa uchumi nchini hivyo basi ipo haja ya kuiunga mkono serikali ya awamu ya Sita ili ukamilike.







***SRG NI UFUPISHO WA NENO LA KIINGEREZA "STANDARD GAUGE RAILWAY" AMBAYO NI RELI YA KISASA YENYE UPANA WA MITA 1.435, AMBAYO INATUMIKA NA NCHI NYINGI DUNIANI KWA ZAIDI YA ASILIMIA 55***

# SGR

**KICHOCHEO CHA UCHUMI TANZANIA**












PICHA TOFAUTI ZIKIONESHA TRENI NA RELI YA KISASA NCHINI CHINA. KUKAMILIKA KWA MRADI WA SGR, KUTAISOGEZA TANZANIA KATIKA VIWANGO HIVI KWENYE SEKTA YA USAFIRISHAJI.

# SGR KICHOCHEO CHA UCHUMI TANZANIA

MAFANIKIO na maendeleo ya nchi yeyote duniani hutazamwa kwa vitu ilivyonavyo na inavyovifanya hasa kwenye mambo yanayomgusa mwananchi moja kwa moja.

Miongoni mwa vitu hivyo ni miundombinu hasa ya usafiri na usafirishaji, nchi yenye miundombinu bora na imara inayoweza kutumika na kufikika nyakati zote za mwaka huwa na nafasi kubwa ya kujiletea maendeleo kwa haraka.

Kwa kiasi kikubwa Tanzania imekuwa ikiendelea kuboresha miundombinu yake ya usafiri na usafirishaji tangu ilipopata uhuru wake Desemba 9, 1961. Itakumbukwa kuwa mwaka 1961 wakati tunapata uhuru wakoloni walituachia kilomita za reli yenye urefu wa kilomita 1245.4 iliyounganisha miji ya Dar es Salaam na Kigoma ikifahamika kama Reli ya Kati, kwa sasa zimefikia zaidi ya Kilomita 2,600 ikijumuisha mikoa ya Tanga na Arusha na kazi inaendelea.

Aidha Serikali imeendelea kuunganisha makao makuu ya mikoa kwa barabara za lami na kazi ya kuifungua nchi kwa njia ya Reli inaendelea. Tanzania ina ukubwa wa kilomita za mraba 950,000, na kutokana na kukua kwa shughuli za kiuchumi, usafiri wa treni umeendelea kufanyiwa maboresho ya mara kwa mara. Shirika la Reli nchini TRC limeendelea kuimarishwa ili kuleta tija iliyokusudiwa tangu lilipoundwa upya mwaka 2017 baada ya Bunge kupitisha muswada wa sheria ya Reli Tanzania ili kuziunganisha kampuni ya Reli Tanzania (TRL) na Kampuni Hodhi ya Rasilimali za Reli (RAHCO ).

## NJIA ZA RELI

Kwa kuzingatia maboresho makubwa yaliyofanywa na serikali kwenye eneo la usafiri na usafirishaji kwa njia ya reli, Jarida la TZ&BEYOND limeiona haja ya kulitazama kwa kina eneo hili.

# MABADILIKO Tabia nchi

**Sote tunapaswa kuwajibika kutunza mazingira kwa minajili ya vizazi vya leo na vya kesho**



Ikumbukwe kuwa wakati tunapata uhuru nchi ilikuwa na njia sita za mtandao wa reli uliokuwa na urefu wa jumla ya kilomita 2,405 na baada ya Uhuru imeweza kuongeza njia mbili ya Ruvu Mruazi na Manyoni Singida ambazo zimefanya jumla ya mtandao wa reli kufikia kilomita 2707.

Lakini pia yapo mafanikio katika eneo hilo kwani kumejengwa mtandao wa reli za TAZARA na ujenzi wa reli ya kisasa yaani SGR ambayo itaunganisha Tanzania na nchi jirani.

TZ&BEYOND inaitazama kwa kina reli hii ya kisasa, ambayo inatajwa kuwa kichocheo kikubwa cha maendeleo ya Tanzania ya sasa na ijayo.

Kwa kuzingatia umuhimu wake tutawadadavulia wasomaji wetu ili wajue SGR ni nini na faida zake ni zipi kwa nchi na kwa mwananchi mmoja mmoja.

### MAANA YA SRG

SRG ni ufupisho wa neno la kiingereza "Standard Gauge Railway" ambayo ni reli ya kisasa yenye upana wa mita 1.435, ambayo inatumika na nchi nyingi duniani kwa zaidi ya asilimia 55.

Tofauti na reli ya kawaida, reli hii inaweza kusafirisha uzito mkubwa na kusafiri kwa mwendo kasi.

### SGR KWA MASLAHI YA TANZANIA

Ili kwenda na kasi ya mabadiliko ya duniani katika eneo la reli, Serikali kupitia shirika la reli Tanzania (TRC) imeazimia kujenga reli hii ya kisasa ili kueneza mtandao usiopungua kilomita 2,561 ikiunganisha mikoa ya Dar es Salaam, Mwanza, Kigoma, Katavi na nchi zisizokuwa na bandari za Rwanda, Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

Uamuazi wa Tanzania kujenga reli hiyo ya SGR unaifanya kuwa nchi ya kwanza Afrika mashariki na Kati kumiliki reli itakayokuwa na uwezo wa kupitisha treni zitakazoendeshwa kwa nishati ya umeme na yenye mwendo kasi usiopungua kilometa 160 kwa saa.

Lengo la reli hiyo ni kuongeza ufanisi katika sekta ya usafiri na usafirishaji nchini.



*IKUMBUKWE KUWA WAKATI TUNAPATA UHURU NCHI ILIKUWA NA NJIA SITA ZA MTANDAO WA RELI ULIOKUWA NA UREFU WA JUMLA YA KILOMITA 2,405*

MWENYEKITI WA BODI YA SHIRIKA LA RELI TANZANIA PROF. JOHN KONDORO (KUSHOTO) AKIWA NA WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI, PROF. MAKAME MBARAWA, KWENYE ENEO LINALOENDELEA KUJENGWA RELI YA KISASA

# MAFANIKIO 7 YA MSINGI

Kutakuwa na ongezeko kubwa la usafirishaji wa mizigo, reli itabeba mzigo wa mpaka tani 10,000 kwa mara moja sawa na uwezo wa maroli 500 ya mizigo, hali hii itasaidia kuzilinda barabara zetu sanjari na kupunguza msongamano wa maroli barabarani.

Kwa kiwango kikubwa kutakuwa na uokoaji wa muda kwa usafiri wa abiria na mizigo na itasaidia kukuza uchumi wa mtu mmoja mmoja na Taifa kwa ujumla.

Vita dhidi ya ukosefu ya ajira inaweza kufanikiwa kwani kutakuwa na ongezeko la ajira kwa wazawa katika sekta na fani mbalimbali.

Kutakuwa na uboreshaji mkubwa wa huduma za kijamii ukihusisha ujenzi wa shule, vituo vya afya na ujenzi wa barabara katika maeneo yanayo pitiwa na mradi.

Reli hii ni kichocheo cha maendeleo katika Nyanja ya kilimo, biashara, madini na viwanda hususan katika maeneo ambayo reli hiyo inapita.

Inamanufaa makubwa kwenye uhusiano wa kimataifa kwani itatuunganisha na nchi jirani za Rwanda, Burundi, Uganda, Kenya na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

Serikali itapunguza mzigo wa ukarabati wa mara kwa mara wa barabara zake.



## AWAMU ZA UJENZI

Ujenzi wa reli ya kisasa wenye mtandao wa km 1,219 za njia kuu, upo katika hatua za mwisho na uligawanyika katika awamu tano muhimu ambazo ni;

- Awamu ya 1 Dae es Salaam – Morogoro (Km 300)
- Awamu ya 2 Morogoro- Makutupora (Km 422)
- Awam ya 3 Makutupora –Tabora (Km 368)
- Awamu ya 4 Tabora – Isaka (Km 130)
- Awaam ya 5 Isaka – Mwanza ( Km 249)
- Awamu ya 6 Uvinza (Kigoma) -Gitega (Burundi)

Awamu ya kwanza: Dar es salaam – Morogoro (Km 300). Ujenzi huu ulizinduliwa na Rais wa Awamu ya Tano, Hayati Dkt. John Magufuli Aprili 12,2017.

Awamu hii ilijumuisha urefu wa kilomita 205 za njia kuu na kilomita 95 za kupishana umekamilika, ulikuwa chini ya mkandarasi YAPI MERKEZI kutoka Uturuki kwa kushirikiana na MOTA ENGIL AFRICA kutoka Ureno.

Awamu hii iligharimu kiasi cha sh. trilioni 2.7 ilijumuisha stesheni sita ambazo ni Dar es Salaam, Pugu, Soga, Ruvu, Ngerengere, Morogoro na kituo cha karakana na treni za mizigo kilichopo Kwala mkoani Pwani.

Mkataba wa ujenzi wa kipande hiki cha kwanza ulisainiwa Februari 3,2017 na ujenzi wake ulianza Mei 2,2017.

Awamu ya pili: Morogoro - Makutupora ( Km 442). Ujenzi wa mradi ulizinduliwa na Rais wa Awamu ya Tano, Hayati Dkt. John Magufuli, Machi 14, 2018.

Ujenzi wa awamu hii uliokuwa na kilomita 336 za njia kuu na kilomita 86 njia za kupishana ulikuwa chini ya mkandarasi YAPI MERKAZI umegharimu kiasi cha sh. trilioni 4.4 ikijumuisha stesheni nane ambazo ni Mkata, Kilosa, Kidete, Gulwe, Igandu, Dodoma, Bahi, Makutupora na kituo cha karakana na treni za mizigo kilichopo Ihumwa mkoani Dodoma.

Kipande cha pili mkataba wake ulisainiwa Septemba 29,2017 na ujenzi wake ulianza Februari 26,2018.

Awamu ya tatu: Makutupora (Singida) -Tabora (Km 368). Utiaji Saini wa mkataba wa ujenzi wa kipande hicho awamu ya tatu ulishuhudiwa na Rais Samia Suluhu Hassan, Desemba 28,2021.

Kipande hiki kina urefu wa kilomita 368 njia kuu ikiwa ni kilomita 294 na njia za kupishana ni kilomita 74, ikiwa na stesheni saba za Manyoni, Itigi, Tura, Malongwe, Goweko, Igalula na tabora.

Gharama ya awamu hii ni sh. trilioni 4.406. Awamu ya 4 : Tabora -Isaka, kipande hiki kinaanzia Tabora hadi Isaka kikiwa na urefu wa kilomita 165, njia kuu ikiwa na urefu wa kilomita 130 na njia ya kupishana ni kilomita 35, kikiwa na stesheni tatu za Nzubuka, Ipala Bukene, Tabora.

Kipande hiki kinagharimu kiasi cha sh. trilioni 2.094

Desemba 20,2022, Rais Samia alishuhudia kwa mara nyengine utiaji saini wa mkataba wa ujenzi wa kipande hicho.

Mkataba huo ulizihusisha pande mbili, upande mmoja ukiwa ni Serikali kupitia Shirika la Reli Tanzania TRC na kampuni za ubia za China Civil Engineering Corporation CECC na China Railways Construction Corporation CRCC.

Utiaji saini huo ulifanyika Ikulu ya Magogoni jijini Dar es salaam, ambapo Rais Samia alibainisha kuwa serikali itaendelea kujenga miradi ya kimkakati kama SGR ili kukuza uchumi. Januari 18,2023,Makamu wa Rais Dkt. Philip Mpango akiwa mkoani Shinyanga , alizindua rasmi ujenzi wa kipande hicho.

Awamu ya 5: Isaka -Mwanza, kipande hiki kinaanzia Isaka hadi Mwanza, kikiwa na urefu wa kilomita 348, njia kuu ikiwa na kilomita 249 na njia za kupishana zikiwa na urefu wa kilomita 92 na stesheni nane za Isaka, Bukene, Shinyanga, Seke, Malampaka, Bukwimba, Mantare, Mwanza Central na kituo cha karakana na treni za mizigo kilichopo Fela mkoani Mwanza.

Mradi huu unagharimu kiasi cha sh. trilioni 3.1 na unatekelezwa kwa ubia kati ya kampuni ya CCECC na CRCC kutoka China.

Awamu ya sita: Uvinza- Gitega, taratibu za kumpata mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa kipande hicho cha reli kitakachoiunganisha Tanzania na Burundi zinaendelea.

Hati ya makubaliano ya ujenzi wa kipande hicho yalishafikiwa Machi 7, 2022 kwa kuzihusisha nchi za Tanzania, Burundi na Jamhuri ya Kidemkrasia ya Congo (DRC).

Makubaliano hayo yalilenga kuuongeza mrandao huo wa reli kutoka Dar es Salaam hadi ufike Kindu -DRC lengo likiwa ni kurahisha huduma ya usafiri na usafirishaji.

Kwa ujumla mradi wote huo hadi kukamilika kwake kwenye vipande vitano utakuwa umegharimu kiasi cha shilingi trilioni 23.3.

**MUUNDO WA SGR**

Reli hii ya kisasa inajengwa sambamba na reli iliyopo sasa ambayo ni ya kawaidi (MGR).

Ujenzi wa uwepo wa reli hii unazingatia uhifadhi wa mazingira na usalama wa watu na mali zao, katika kuhakikisha hilo linafanyika yapo mambo matatu yamezingatiwa ambayo ni :-

**1** KUWEKWA KIVUKO CHA JUU NA CHINI KILA KWENYE SEHEMU ZA MWINGILIANO WA MAGARI NA RELI.

**2** KUMEJENGWA UZIO KWA USALAMA WA WATU NA WANYAMA.

**3** ELIMU IMEENDELEA KUTOLEWA KWA WANANCHI KUHUSIANA NA USALAMA KWA UJUMLA.

**FIDIA KWA WENYE ARDHI**

Kwa kuzingatia utawala wa sheria na kuheshimu wananchi wake serikali imeendelea kusimamia sheria na taratibu zote katika kufanikisha ujenzi huo.

Hivyo basi kwa mujibu wa sheria ya ardhi ya mwaka 1999 na sheria ya tathmini ya mwaka 2016, maeneo yote yaliyo pitiwa na mradi huo na hayakuwa mali ya TRC yalifanyiwa tathmini na kuwalipa wamiliki stahiki zao.



Kukamilika kwa mradi huo kutapunguza muda wa safari, ambapo msafiri atatumia saa sita kutoka Dar es Salaam kwenda Tabora.

Gharama ya awamu hii ni sh. trilioni

**4.406**

kipande hiki kinaanzia Tabora hadi Isaka kikiwa na urefu wa kilomita 165, njia kuu ikiwa na urefu wa kilomita 130 na njia ya kupishana ni kilomita 35, kikiwa na stesheni tatu za Nzubuka, Ipala Bukene, Tabora.

KIPANDE HIKI KINAGHARIMU KIASI CHA SH. TRILIONI 2.094








TRC NA MAENDELEO YA

# SGR



KITUO KIKUU CHA TRENI YA KISASA KILICHOPO JIJINI DAR ES SALAAM




RAIS SAMIA SULUHU HASSAN, AKIKATA UTEPE KUASHIRIA UZINDUZI WA UJENZI WA RELI YA KISASA KIPANDE CHA KUTOKA MWANZA HADI ISAKA, KM 341

TRC NA MAENDELEO YA

# SGR

SHIRIKA la Reli Tanzania ndie msimamizi mkuu wa mradi wa ujenzi wa Reli ya Kisasa (SGR), lenyewe ndio linabeba na kuhifadhi taarifa zote zinazohusiana na mradi huo ambao ni wa kimkakati kutokana na umuhimu wake kwa nchi na wananchi.

Kutokana na umuhimu wa mradi huo TRC kupitia kwa Mtendaji Mkuu wake, Masanja Kadogosa imekuwa ikitoa taarifa za mara kwa mara za maendeleo ya mradi huo.

Kwenye mradi huu Kadogosa amekuwa mstari wa mbele kutoa taarifa wakati wowote zinapohitajika.

Alianza kufanya hivyo tangu kuanza kwa mradi huo ambao kwa ujumla wake unaiunganisha mikoa ya Dar es Salaam na Mwanza ikijumlisha urefu wa kilomita zaidi ya 1000, kwa njia kuu iliyogawanywa katika vipande vitano vya Dae es Salaam – Morogoro (Km 300),Morogoro- Makutupora (Km 422), Makutupora – Tabora (Km 294), Tabora – Isaka (Km 130) na Mwanza ( Km 249).

Katika mazungumzo yake na jarida hili, Kadogosa ambaye kimsingi ni mchapakazi asiye choka alielezea umuhimu wa mradi huu kuwa ukikamilika utachochea mipango ya maendeleo ya Serikali sanjari na kuchochea mapinduzi ya kiuchumi kwa kanda nzima ya Afrika Mashariki na Kati hususani nchi zisizopakana na Bahari.

**MPANGO KAZI**

Akielezea muda wa mradi Kadogosa alisema kwa kiasi kikubwa mradi unakwenda vizuri na kwa wakati kulingana na mpango kazi uliopo.

> ***RELI HII ITACHOCHEA MAPINDUZI YA KIUCHUMI KWA KANDA NZIMA YA AFRIKA MASHARIKI NA KATI HUSUSANI NCHI ZISIZOPAKANA NA BAHARI.***

***VIPANDE VIWILI VYA KWANZA VYA MRADI HUO VILIIGHARIMU SERIKALI JUMLA YA SHILINGI TRILIONI 7.1 AMBAZO NI PESA ZA WALIPA KODI WA TANZANIA.***

TRENI ZITAENDESHWA KWA KUTUMIA NISHATI YA UMEME KUTOKA TANESCO.

Alisema kipande cha kutoka Dar es Salaam hadi Makutupora (Singida) tayari kimekamilika kama kilivyopangwa kukamilika.

“Utekelezaji wa kipande cha kwanza kati ya Dar es salaam na Morogoro kilisainiwa Februari 3, 2017, ujenzi wake ulianza Mei 2, 2017 na kilipangwa kukamilika Novemba 2, 2019 na kipande cha Morogoro -Makutupora mkataba wake ulisainiwa Septemba 29, 2017 na ujenzi ulianza Februari 26, 2018 na kilipangwa kukamilika Februari 25, 2021, jambo la kufurahisha ni kwamba vipande vyote hivi vimeshakamilika.”

## KILOMITA ZA UJENZI

Akizungumzia suala la wakandarasi wa mradi huo, Kadogosa alisema jumla ya Kilomita 722 za ujenzi wa reli katika vipande viwili, kipande cha Dar es Salaam-Morogoro kilomita 300 kimejengwa kwa ubia wa kampuni ya Yapi Markezi ya Uturuki na Mota-Engil ya Ureno na kipande cha Morogoro Makutupora chenye kilomita 422, kipande cha Makutupora-Tabora chenye urefu wa kilomita 368 na Tabora- Isaka chenye urefu wa kilomita 165 kwa pamoja vinajengwa na mkandarasi Yapi Markez, huku kipande cha Isaka-Mwanza chenye urefu wa kilomita 348 kikijengwa kwa ubia kati ya kampuni ya CCECC na CRCC kutoka China.

## WAANGALIZI

Kadogosa aliwataja wasimamizi wa mradi huo kuwa ni Mhandisi Mshauri anayesimamia kwa niaba ya Serikali ambayo ni kampuni ya Korail Jv ambayo ni ubia wa Kampuni nane za Korail, Cheil na DMEC kutoka Korea, Multitech kutoka Botswana, Unitec kutoka Tanzania, Baraji kutoka India, SSF kutoka Ujerumani na RINA kutoka Italia

## GHARAMA ZA MRADI

Kwa mujibu wa Kadogosa, vipande viwili vya kwanza vya mradi huo viligharimu serikali jumla ya shilingi Trilioni 7.1 ambazo ni pesa za walipa kodi wa Tanzania.

## CHANGAMOTO

Kadogosa alizitaja changamoto zilizoukabili mradi huo kuwa ni pamoja na kupita kwenye maeneo mbalimbali ya nchi yenye milima, mabonde, misitu na maeneo ya watu.



FUNDI AKIUNGANISHA VIPANDE VYA RELI KATIKA ENEO LA RUVU, MKOANI PWANI






*JUMLA YA STESHENI SITA ZIMEJENGWA KATI YA DAR ES SALAAM NA MOROGORO, KATI YA HIZO STESHENI KUBWA NI MBILI NA STESHENI  NDOGO NI NNE.*



MWONEKANO WA TRENI YA KISASA NCHINI CHINA. MOJA YA NDOTO ZA SERIKALI YA TANZANIA NI KUPUNGUZA GHARAMA ZA USAFIRISHAJI KWA KUTUMIA TRENI ZA KISASA KAMA ILIVYOFANIKIWA CHINA.

**TAYARI KUNA KARAKANA KUBWA NA KITUO KIKUU CHA KUUNGANISHIA TRENI ZENYE UREFU WA KILOMETA MBILI**



MOJA YA TRENI ZA KISASA ZINAZOTUMIKA NCHINI MISRI, TANZANIA SASA INAELEKEA KWENYE USAFIRI WA AINA HII

Ili kufanikisha kulikuwa na ukataji wa milima na ujazaji wa mabonde (Earthworks), na kwamba tayari jumla ya mita za ujazo milioni 23.4 za kifusi zilikatwa.

### MADARAJA

Alisema kimsingi kazi kubwa ya ujenzi wa madaraja na makalavati imekamilika na kwamba daraja refu ni lile lililopo katikati ya jiji la Dar es salaam ambalo lina jumla ya Kilomita 2.56. Lakini pia kuna madaraja ya kati 26 na Makalavati 243, Madaraja ya Treni kupita juu 17, Madaraja ya treni kupita chini 15 na Madaraja ya reli juu ya reli (rail over rail) matano.

### STESHENI

Kadogosa alisema mradi huo utahusisha stesheni nyingi ambapo katika kipande cha kwanza stesheni sita zimejengwa kati ya Dar es salaam na Morogoro, kati ya hizo stesheni kubwa ni mbili na stesheni ndogo ni nne. Usanifu wa Stesheni hizo umezingatia mazingira na asili ya Tanzania ambapo stesheni ya Dar es Salaam ina sura ya madini adimu ya Tanzanite wakati stesheni za kati ujenzi wake umezingatia utamaduni na nyumba zetu za asili. Stesheni ya Morogoro inaonesha uhalisia wa milima ya Uruguru.

### MFUMO WA UENDESHAJI

Akizungumzia mfumo wa uendeshaji alisema treni zitaendeshwa kwa kutumia nishati ya umeme kutoka Tanesco.

### MFUMO WA MAWASILIANO

Mfumo wa Kisasa zaidi uitwao European Train Control System Level 2 utatumika na kuongeza ufanisi wa uendeshaji na usalama wa treni ambapo treni zitaongozwa kupitia kituo maalum (Central Train Control).

### KARAKANA KUU

Tayari kuna karakana kubwa na Kituo kikuu cha kuunganishia treni zenye urefu wa kilometa mbili kilichopo katika eneo la Kwala wilayani Kibaha.

Lengo la kituo hiki ni kuunganisha shughuli za reli na bandari kavu (ICD) iliyoko eneo hilo na kupunguza msongamano wa magari makubwa yaingiayo na kutoka jijini Dar es salaam.

Aidha kituo hiki kitaongeza ufanisi wa kuingiza na kuondoa mizigo katika bandari ya Dar es salaam ambapo mizigo itachukuliwa na treni fupi fupi ambazo zitaunganishwa hadi kuwa na urefu wa kilomita mbili katika kituo hiki cha Kwala kabla ya kuendelea na safari zake kuelekea mikoani na nchi jirani.





WAZIRI MKUU KASSIM MAJALIWA, ALIPOTEMBELEA KAMPUNI INAYOTENGENEZA MABEHEWA NA INJINI ZA TREN YA SGR, NCHINI KOREA KUSINI

**MATARUMA YALIYOTUMIKA KATIKA MRADI HUU NI 500,100 KWA KIPANDE CHA DAR ES SALAAM – MOROGORO WAKATI KWA KIPANDE CHA MOROGORO – MAKUTUPORA YAMETUMIKA MATARUMA 703,300. MATARUMA YOTE HAYA YANATENGENEZWA HAPA NCHINI KATIKA ENEO LA MRADI**

### UTANDIKAJI RELI

Utandikaji wa reli unaendelea kwenye vipande vinavyoendelea kujengwa, hata hivyo katika awamu ya kwanza zilitandikwa zaidi ya Kilomita 10 pamoja na kuletwa kwa tani 7,250 za reli sawa na urefu wa kilometa 60.

Mataruma yaliyotumika katika mradi huu ni 500,100 kwa kipande cha Dar es salaam – Morogoro wakati kwa kipande cha Morogoro – Makutupora yametumika mataruma 703,300. Mataruma yote haya yanatengenezwa hapa nchini katika eneo la mradi.

Kwa awamu ya kwanza pekee kiwanda cha mataruma kilichoko Soga - Kibaha kilizalisha zaidi ya mataruma 27,000 ambayo ni sawa na asilimia 5.4%.

### AJIRA

Kadogosa alisema katika hatua ya awali mradi huo uliajiri jumla ya wafanyakazi 5,440, vibarua 4,743 na kwamba watanzania walikuwa sawa na asilimia 96% na asilimia nne ni walikuwa ni wageni, wataalamu 189 wa kitanzania na 258 wa kigeni kwa uwiano wa 42% watanzania na 58% wageni.

Hata hivyo mkataba ulimtaka mkandarasi kuwa na uwiano wa 20% watanzania na 80% wageni kwenye kada ya wataalamu ambapo mpaka sasa amevuka kiwango hicho kwa kuwashirikisha watalamu wengi wa kitanzania moja kwa moja.

Kwa upande wa wafanyakazi wasio na utaalamu (semi-skilled) kimkataba uwiano ulikuwa 80% watanzania na 20% wageni lakini mpaka sasa mkandarasi amevuka uwiano huo kwa kuwashirikisha watanzania kwa asilimia 96% Pia jumla ya ajira 626 za watanzania wasio na utaalamu na 19 za wenye utaalamu zimepatikana kupitia kampuni za wazawa (Sub-Contractors) wanaoshiriki moja kwa moja kwenye mradi huu.

### ATHARI ZA MRADI

Ardhi na mali nyingine za wananchi wapatao 6,514 zenye thamani kiasi cha shilingi za kitanzania billion 83.099 zilihamishwa ili kupisha ujenzi wa Reli kwa kipande cha Dar es Salaam-Morogoro.

### UJENZI WA TUTA

Ujenzi wa tuta umeshafanyika na jumla ya kilometa 80 zilisafishwa,hii ilikuwa ni kwenye kipande cha kwanza.



WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI, PROF. MAKAME MBARAWA AKIKAZA KIUNGIO CHA RELI KATIKA ENEO LA KWALA, MKOANI PWANI







TRENI YA KISASA AMBAYO IMECHANGIA KUBADILI MWONEKANO WA JIJI LA CANBERRA, NCHINI AUSTRALIA

**FAIDA ZA MRADI HUO ZIMEGAWANYIKA KATIKA SEHEMU ZIFUATAZO:**

1. WAKATI WA UJENZI UNAPOENDELEA

UMEWEZA KUCHANGIA PATO LA TAIFA, KUMEKUWA NA MAHITAJI MAKUBWA YA SARUJI, KOKOTO, NONDO PAMOJA NA VIFAA VINGINE VYA UJENZI HIVYO KUVIFANYA VIWANDA VYETU VYA NDANI KUPATA SOKO LA BIDHAA ZAKE.

SEKTA YA USAFIRISHAJI PIA IMEFAIDIKA, KUNA BAADHI YA WATANZANIA WAMEKODISHA MAGARI YAO PAMOJA NA KUSHIRIKI MOJA KWA MOJA KATIKA USAFIRISHAJI WA VIFAA NA MITAMBO MBALIMBALI.

BAADHI YA WAKANDARASI WAZAWA WANASHIRIKI MOJA KWA MOJA KUTOA HUDUMA ZA UJENZI.

KATIKA KUPITIA ONGEZEKO LA MAHITAJI YA VIFAA VYA UJENZI AJIRA NYINGINE ZIMEZALISHWA KWENYE VIWANDA HIVYO

KWA AWAMU YA KWANZA MRADI UMETOA ZAIDI YA AJIRA 5,440 ZA MOJA KWA MOJA.

**MRADI UTAKAPOKAMILIKA UTAKUWA NA FAIDA ZIFUATAZO:**

KUCHOCHEA UANZISHWAJI WA VIWANDA MAENEO MENGINE YA NCHI NA KUTOA UHAKIKA WA USAFIRISHAJI WA MALI GHAFI NA BIDHAA.

MRADI UTACHOCHEA UANZISHWAJI WA MIJI MIDOGO KATIKA SEHEMU ZINAZOJENGWA STESHENI AMBAZO ZITAKUWA KIVUTIO KWA WANANCHI, MFANO MAENEO YA SOGA, RUVU NA KWALA MKOANI PWANI.

KUONGEZA UFANISI WA USAFIRISHAJI WA ABIRIA NA MIZIGO KWA KUPUNGUZA MUDA WA SAFARI MATHALANI DAR ES SALAAM-MOROGORO SAFARI ITATUMIA SAA MOJA NA DAKIKA 15, SAFARI YA DSM – DODOMA MUDA WA SAFARI UTAKUWA SAA TATU.

UTAPUNGUZA GHARAMA ZA USAFIRISHAJI MIZIGO, MRADI UTAKAPOANZA GHARAMA ZA USAFIRISHAJI WA MIZIGO ITASHUKA KWA ASILIMIA 40%.



MUONEKANO WA KARAKANA YA RELI YA KISASA SGR KATIKA ENEO LA KWALA







***MRADI UTACHOCHEA UANZISHWAJI WA MIJI MIDOGO KATIKA SEHEMU ZINAZOJENGWA STESHENI AMBAZO ZITAKUWA KIVUTIO KWA WANANCHI, MFANO MAENEO YA SOGA, RUVU NA KWALA KWA MKOA WA PWANI.***

MUONEKANO WA RELI YA KISASA KATIKA ENEO LA STESHENI YA MOROGORO

# SGR FURSA KUBWA YA KIUCHUMI

KAZI IENDELEE hii ni kauli mbiu ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Samia Suluhu Hassan ambayo yeye mwenyewe pamoja na wale aliowapa dhamana wanaisimamia kwa vitendo.

Tangu Rais Samia aingie madarakani Machi 19,2021 amekuwa muwazi na mwenye kumpa mwananchi matumaini ya kweli huku akiahidi kuendeleza kwa kiwango cha juu miradi yote iliyoachwa na mtangulizi wake, hayati Dkt. John Magufuli pamoja na kuanzisha mipya.

Katika kuthibitisha hilo amefanikiwa kuusimamia kikamilifu mradi wa ujenzi wa Reli ya Kisasa (SGR) ambao sasa unakwenda kwa kasi kubwa.

Katika kudhihirisha kuwa hatanii alianza kusimamia kauli yake ya Kazi iendelee kwa kuweka jiwe la msingi la ujenzi wa Reli ya Kisasa kipande cha Mwanza – Isaka.

Alifanya hivyo wakati wa ziara yake ya kikazi jijini Mwanza, ambapo pamoja na mambo mengine alizindua na kuasisi miradi mbalimbali ya maendeleo.

Akihutubia wakati wa uwekaji wa jiwe la msingi la mradi huo wa ujenzi wa reli ya kisasa ya Mwanza - Isaka yenye urefu wa kilometa 341 ambao unagharimu kiasi cha shilingi Trilioni 3.06, alisema mradi huo utaongeza kasi ya ukuaji wa uchumi kwa kusafirisha kwa haraka na kwa kiwango kikubwa cha mizigo na watu tofauti na ilivyo sasa.

"Mradi huu ni sehemu ya mradi mkubwa wa reli kutoka Dar es Salaam hadi Mwanza yenye urefu wa kilomita 1,605 ambao utatengeneza ajira 11,000 hivyo niwaombe wananchi wa Mwanza mchangamkia fursa ya ujenzi wa reli hiyo kwa kuwa wavuvi, wakulima na wafugaji watanufaika na reli hiyo ambayo itakuwa na mabehewa maalum ya kubebea mazao, nyama na samaki."

Aidha alisema reli hiyo itapunguza muda wa kusafiri kati ya Mwanza hadi Dar es Salaam kutoka saa 17 za sasa kwa usafiri wa mabasi hadi saa 8 mradi utakapokamilika.

### KAULI YA KADOGOSA

Katika hafla hiyo Mkurugenzi Mkuu wa TRC, Masanja Kadogosa alisema mkataba huo unahusisha ujenzi wa reli ya SGR kipande cha kuanzia Makutopora hadi Tabora chenye urefu wa kilomita 368 kwa gharama ya dola bilioni 1.98 ambazo ni sawa na shilingi trilioni 4.4 na ujenzi huo utachukua miezi 46.



MAENDELEO SGR

## WAZIRIMKUU: MRADI UTAKAMILIKA KWA WAKATI

MAENDELEO YA UJENZI HUU YANATIA MATUMAINI

KAZI INAENDELEA KWA UFANISI

"Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan amedhamiria kukamilisha ujenzi wa miradi yote iliyoanzishwa, hivyo Watanzania waendelee kuwa na imani na Serikali yao, na tunawahakikishia mradi huu utakamilika kwa wakati." Hiyo ni kauli ya Waziri Mkuu Kassim Majaliwa aliyoitoa wakati akikagua maendeleo ya ujenzi wa mradi wa Reli ya Kisasa (SGR) katika kituo cha Kwala kilichopo mkoani Pwani, ambacho kitatumika kama kituo kikuu cha kufanya matengenezo makubwa ya mabehewa na injini za treni. "Maendeleo ya ujenzi huu yanatia matumaini na kazi inaendelea kwa ufanisi na maeneo yaliyobaki yatakamilika kwa wakati, nimeridhishwa na vituo vya abiria vilivyokamilika." Aidha, Waziri Mkuu aliwasihi wafanyakazi wa mradi huo kufanya kazi kwa ufanisi kwani lengo la Serikali ni kuufikisha mradi huo katika mikoa ya Mwanza, Kigoma na Katavi katika bandari ya Karema. "Njia zote za reli tunataka ziwe za kisasa, hii pia itawezesha kuinua uchumi wa mtu mmoja mmoja na taifa kwa ujumla, nchi yetu ni ya kimkakati kwa sababu nchi zote za jirani zinategemea reli hii." Aliongeza kuwa kukamilika kwa mradi huo kutaongeza ufanisi wa usafirishaji wa abiria na mizigo kwa kupunguza muda wa safari, kutoka Dar es Salaam, Morogoro, Dodoma na Mwanza.

**Njia zote za reli tunataka ziwe za kisasa, hii pia itawezesha kuinua uchumi wa mtu mmoja mmoja na taifa kwa ujumla, nchi yetu ni ya kimkakati kwa sababu nchi zote za jirani zinategemea reli hii**

WAZIRI MKUU,
KASSIM MAJALIWA





MUONEKANO WA MAJENGO YA KARAKANA YA RELI YA KISASASA MKOANI PWANI

ELIMU YA MAZINGIRA

# JET YAWANOA WAANDISHI JUU YA MASUALA YA SHOROBA

NA SIDI MGUMIA, BAGAMOYO

KATIKA kufanikisha ushiriki wa wanahabari kwenye masuala ya maendeleo ya nchi Chama cha Waandishi wa Habari za Mazingira Tanzania (JET), kimeiona haja ya kuwapa mafunzo waandishi wa habari 25 ili wajue namna sahihi ya kuripoti masuala yanayohusu mapito ya Wanyama maarufu kama ushoroba.

Mafunzo hayo yaliyoratibiwa na JET kwa ufadhili wa Shirika la Marekani la Maendeleo ya Kimataifa (USAID) kupitia mradi wake wa Tuhifadhi Maliasili yamefanyika Bagamoyo mkoani Pwani Januari 12-13,2023.

Akizungumza na waandishi wa habari kwenye ufunguzi wa semina hiyo Mkurugenzi wa JET, John Chikomo alisema mafunzo hayo ni muhimu kwa waandishi kwakua wengi hawana uelewa na elimu ya shoroba.

"Ni vyema kwa waandishi kuelewa kwa undani mausala ya shoroba ili kuandika habari kwa kina na iwe rahisi kufikisha ujumbe kwa ufasaha kwa jamii, hivyo kupitia semina hii waandishi watafahamu faida zinazotokana na uhifadhi na utunzaji wa hizo shoroba,"alisema Chikomo.

Ameongeza kuwa katika mapambano dhidi ya changamoto za mabadiliko ya tabia nchi elimu ya mazingira na haswa uhifadhi bado inahitaji iepelekwe kwenye jamii lakini pia kusisitiza uwepo wa ushirikishwaji wa sekta na wizara mbalimbali katika masuala ya mazingira.

Pamoja na hilo, Chikomo alisisitiza kuwa ongezeko la watalii wanaoingia nchini ni mafanikio yanayotokana na elimu ya uhifadhi wa mazingira na wanyamapori inayotolewa kwa waandishi wa habari ambao wanaifikisha kwa jamii. Nae Dk. Elikana Kalumanga ambaye ni Meneja Ushirikishwaji wa Sekta Binafsi wa Mradi wa Shirika la Marekani la Maendeleo ya Kimataifa (USAID) wa Tuhifadhi Maliasili alisema kwa sasa hali za shoroba mbalimbali nchini si nzuri na kwa mujibu wa takwimu za serikali zipo baadhi zimepotea kabisa kutokana na shughuli zinazofanywa na wananchi.



WANAHABARI WAKIPATA MAFUNZO

Akifafanua juu ya changamoto za migogoro ya binadamu na wanyamapori John Steven Noronha, Meneja Ufuatiliaji na Tathmini wa Mradi wa Shirika la Marekani la Maendeleo ya Kimataifa (USAID) wa Tuhifadhi Maliasili alisema migogoro hiyo ni kikwazo kikuu cha kuunganisha uhifadhi na kupunguza umaskini, kwani gharama za kuishi na wanyamapori huathiri vibaya maisha ya vijijini na kuzorotesha usaidizi wa jamii kwa ajili ya uhifadhi. Kwa upande wake Mwenyekiti wa JET, Dk. Ellen Otaru alisema anaamini semina hiyo itakuwa na faida kubwa kwa waandishi wa Habari.



TZ&BEYOND



***Jarida hili linalowafikia watu wa rika na kada*** mbalimbali ndani na nje ya Tanzania limelenga kukupa maarifa ambayo huwezi kuyapata kwenye jarida lolote **Tanzania**.

**TZ&BEYOND** limejikita kwenye kuchambua masuala ya siasa, Bunge, Uchumi, Mazingira, Uhifadhi na Habari za kimataifa dhamira yake kuu ni kuwa darasa mikononi mwako.

***TUNA MWANZO, HATUNA MWISHO***

USIKOSE KUSOMA MAJARIDA YETU KUPITIA TOVUTI

www.tz&beyond.co.tz

MAENDELEO SGR

## RAIS SAMIA: RAIS SAMIA: SITAKUBALI FEDHA ZA SGR ZIPOTEE

UJENZI WA RELI YA KISASA (SGR) KUTOKA DAR ES SALAAM HADI MWANZA UKAMILIKE

KIPAUMBELE KITOLEWE KWA YALE MATAWI YANAYOTUUNGANISHA NA NCHI ZA JIRANI

Rais Samia Suluhu Hassan amewahakikishia Watanzania kuwa kwa vyovyote itakavyokuwa ni lazima ujenzi wa reli ya kisasa (SGR) kutoka jijini Dar es Salaam hadi mkoani Mwanza ukamilike kwa wakati na fedha zitakazotumika ni mikopo yenye masharti nafuu na atakopa ili kuhakikisha fedha zilizokwisha wekezwa kwenye mradi huo hazipotei.
Rais Samia amekuwa akiirejea kauli hiyo mara kwa mara na hata aliposhuhudia utiaji saini mkataba wa ujenzi kati ya Shirika la Reli la Tanzania (TRC) na Kampuni ya Yerpi Merkezi ya nchini Uturuki kwaajili ya ujenzi wa reli wa kipande cha kilometa 368 yenye gharama ya dola za kimarekani bilioni 1.908. Rais Samia alisema reli hiyo ina umuhimu mkubwa katika uchumi wa nchi kwa sababu itarahisisha usafirishaji wa abiria na mizigo ndani na nje ya nchi, hivyo lazima ijengwe kama ilivyokusudiwa. Kiongozi huyo mkuu wa nchi amebainisha kuwa uwekezaji wa ujenzi wa vipande vinne kati vitano vya awamu ya kwanza ya ujenzi wa reli hiyo umefikia kiasi cha Sh14.7 trilioni ukijumuisha na kodi na kwamba hatakubali fedha hizo zipotee bure kwa mradi kushindwa kukamilika.
"Tusipoendelea na reli hakutakuwa na faida, fedha tulizozilaza pale chini zitakua hazina maana, ni lazima Serikali ikope fedha nje kukidhi mahitaji ya mradi huo.
"Kwa hiyo kwa njia yoyote kwa vyovyote tutakopa, tutaangalia njia rahisi zitakazotufaa za kukopa kwa sababu fedha hizi hatutazitoa kwenye tozo wala kwenye kodi tunazokusanya ndani."
Kuhusu kupata mkopo, Rais Samia alisema "Niwaombe ndugu zangu mnaosimamia hii sekta twendeni, mimi niko pamoja nanyi tutasimama kuangalia mikopo inayotufaa tukiongozwa na Gavana wa Benki Kuu na Waziri wa Fedha yuko hapa atatuongoza mikopo gani itatufaa tutachukua tumalize reli hii ndani ya muda uliopangwa ili iweze kutengeneza fedha tulipe mikopo tunayochukua." Reli hiyo ya kisasa inajengwa na Yerpi Markezi ambaye anajenga vipande vitatu kati ya vitano vya reli hiyo yenye mtandao usiopungua kilomita 2,561 ikiunganisha mikoa ya Dar es Salaam, Mwanza, Kigoma, Katavi na nchi zisizokuwa na bandari (Rwanda, Burundi na Congo DRC).
"Nitoe maelekezo kwamba tunapokwenda kumaliza (reli ya SGR) kipaumbele kitolewe kwa yale matawi yanayotuunganisha na nchi za jirani ili tuweze kurahisisha biashara zetu, kuingia kwenye masoko kwa urahisi."

**Uwekezaji wa ujenzi wa vipande vinne kati vitano umegharimu kiasi cha Sh14.7 trilioni**

RAIS DKT.
SAMIA SULUHU HASSAN

TUSIPOENDELEA NA RELI
HAKUTAKUWA NA FAIDA,
FEDHA TULIZOZILAZA PALE
CHINI ZITAKUA HAZINA
MAANA, NI LAZIMA SERIKALI
IKOPE FEDHA NJE KUKIDHI
MAHITAJI YA MRADI HUO.





*RAIS SAMIA ALISEMA RELI HIYO INA UMUHIMU MKUBWA KATIKA UCHUMI WA NCHI KWA SABABU ITARAHISISHA USAFIRISHAJI WA ABIRIA NA MIZIGO NDANI NA NJE YA NCHI*

PICHA YA TRENI ZA KISASA INAYOTUMIWA KUSAFIRISHA ABIRIA NCHINI KOREA KUSINI. DHAMIRA YA SERIKALI YA TANZANIA NI KUHAKIKISHA NCHI INAFIKIA HATUA HII KWA LENGO LA KUHARAKISHA MAENDELEO








MAKAMU WA RAIS DKT. PHILIP MPANGO AKIWA PAMOJA NA WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI PROF. MAKAME MBARAWA PAMOJA NA VIONGOZI WENGINE WA CHAMA NA SERIKALI AKIWEKA JIWE LA MSINGI UJENZI WA RELI YA KISASA (SGR) KIPANDE CHA NNE TABORA – ISAKA







MAKAMU WA RAIS DKT. PHILIP MPANGO AKISIKILIZA MAELEZO KUTOKA KWA MKURUGENZI WA SHIRIKA LA RELI TANZANIA (TRC) MASANJA KADOGOSA WAKATI AKITEMBEA KATIKA MFANO WA RELI YA KISASA (SGR) KIPANDE CHA NNE TABORA – ISAKA



TIPER

TANZANIA INTERNATIONAL PETROLEUM RESERVES L.T.D




TIPER
BULK STORAGE



**TIPER** the joint venture company between the government of Tanzania and Oryx Energies SA (OESA) based in Geneva with equal shares 50% each operates the largest storage facility for petroleum in the country. Current storage capacity is 253.7 million litres.

TIPER which used to be known as Tanzanian Italian Petroleum Refining (TIPER) Company Limited, commissioned refinery business in 1966. In year 2000, the refinery business ceased. In 1999 Agippetrol International (BV) - "Agip" sold its assets in TIPER as well as the 50% shareholding of the company to Oryx Energies SA., GENEVA (OESA). The remaining 50% shares continued to be owned by the Government of Tanzania.

Following the liberalization of the downstream petroleum subsector in Tanzania, TIPER found it uneconomical to operate as a refinery. In mid-2000, the company changed its main objective from refining to petroleum product storage. The refinery was decommissioned, scrapped and the plant was then converted in to a refined petroleum storage terminal, whose core business is the bulk storage and handling of refined petroleum products with delivery of the customer's product through cross pumping to other terminals, back-loading for onward transshipment and truck loading for onward sale at local commercial and retail outlets as well as for transit.








**TIPER** operating as a bulk liquid storage entity, stores low sulphur diesel (AGO), Premium Motor Spirit " (PMS), Dual Purpose Kerosene (DPK) and Heavy Fuel Oil (HFO 180) which is widely used in industrial applications. TIPER operating as storage facility has facilitated to a greater extent the availability of petroleum products in the country as well as for neighboring land locked countries.

## TIPER'S CURRENT STORAGE CAPACITY BY PRODUCT IS SHOWN BELOW:

| Product | Capacity (Litres) |
|---|---|
| Diesel (AGO) | 180,246,000 |
| Premium Motor Spirit " (PMS) | 56,302,000 |
| Dual Purpose Kerosene (DPK) | 5,723,000 |
| HFO 180 | 11,383,000 |
| Total Storage Capacity | 253,654,000 |



# TIPER's *future* plan include:










# BEHEWA MPYA ZA SGR ZIMEWASILI

UJIO wa mabehewa mapya 14 ya reli ya kisasa -SGR yameunogesha mradi huo ambao unatajwa kuwa mwarubaini wa usafiri na usafirishaji nchini.

Novemba 25,2022 ndani ya viunga vya bandari ya Dar es Salaam, kulifanyika hafla ya kuyapokea mabehewa hayo. Shirika la Reli Tanzania – TRC ndio lilikuwa mpokeaji wa behewa hizo zilizonunuliwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ajili ya uendeshaji wa reli ya kisasa nchini.

Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi Prof. Makame Mbarawa alisema ujenzi wa reli ya kisasa - SGR unakwenda sambamba na ununuzi wa Behewa na vichwa vya treni kwaajili ya utoaji wa huduma katika reli ya kisasa.

Behewa hizo 14 ni kati ya 59 zilizotengenezwa na kampuni ya Sun Shin Rolling Stock Technology Limited (SSRST) iliyopo nchini Korea ya Kusini. Tayari serikali imeshatoa Dola za Marekani million 295.74 kwa kampuni ya Hyundai Rotem ya Korea Kusini kwaajili ya ununuzi wa vichwa vya treni vya umeme 17 na seti za treni za kisasa (Electric Multiple Unit - EMU) 10 na 'locomotive simulator' moja ya umeme, pia kuna behewa 1,430 za mizigo ambazo ziko katika matengenezo.

**MAKAME MBARAWA ALISEMA UJENZI WA RELI YA KISASA – SGR UNAKWENDA SAMBAMBA NA UNUNUZI WA BEHEWA NA VICHWA VYA TRENI KWAAJILI YA UTOAJI WA HUDUMA KATIKA RELI YA KISASA**

WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI
PROF. MAKAME MBARAWA






Prof. Mbarawa alitoa ufafanuzi kuhusu aina ya treni zinazokuja nchini Tanzania, "Serikali imeagiza vichwa vya treni ya umeme kwaajili ya kuvuta behewa hizi, katika treni za umeme kuna vichwa vya treni aina tatu ambavyo ni 'Electric Locomotive' kazi yake ni kuvuta behewa kama hizi 14 zilizokuja, 'Electric Multiple Unit' (EMU) kichwa cha treni ya aina hii kimeungwa na behewa pamoja, na aina ya tatu kichwa cha treni ni kile ambacho kinatumika mahususi kwa ajili ya mwendo kasi wa hali ya juu".

Prof. Mbarawa aliweka wazi kuwa "kwenye utaratibu wa treni za umeme, treni inayokwenda mwendokasi zaidi ya Kilomita 200 kwa saa inaitwa ya mwendokasi, na zile treni ambazo mwendo wake ni chini ya Kilomita 200 kwa saa zinaitwa treni za kawaida. Hivyo treni yetu ya Tanzania ni treni ya umeme ya kawaida inayokwenda Kilomita 160 kwa saa".

### KOREA KUSINI YAFURAHIA

Balozi wa Korea Kusini nchini Tanzania Kim Sun Pyo alifurahia hatua hiyo na kusema ni ya kihistoria kwa Tanzania na Nchi ya Korea Kusini.

Balozi Kim ameweka wazi hatua ya kuleta behewa za SGR nchini Tanzania ni ya kupongezwa, kwani mradi huo wa SGR utasaidia kukuza uchumi wan chi. Amesisitiza kuwa Korea Kusini itaendelea kutoa ushirikiano katika kusaidia mradi wa SGR, sanjari na kutoa pongezi kwa Serikali na TRC kwa ujenzi wa SGR ambao utarahisisha usafiri na usafirishaji nchini.

### KADOGOSA NA GHARAMA ZILIZOTUMIKA

Mkurugenzi Mkuu TRC Masanja Kadogosa ameeleza gharama zilizotumika katika utengenezaji wa behewa hizo, "mkataba wa utengezaji wa Behewa hizi 59 ambazo behewa 14 tumeshazipokea umegharimu Dola za Kimarekani 55.6, muda wa mkataba ulikuwa miaka miwili ambao unahusisha utengenezaji wa behewa za daraja la juu (Business class) na daraja la chini (Economy class), kusafirisha, kufanya majaribio na mafunzo kwa ajili ya wasimamizi wetu kupitia TRC.

Kwa taarifa tulizonazo mpaka sasa utengenezaji wa behewa zilizobaki umefikia asilimia 86 na mwezi Mei 2023 tutakuwa tumepokea behewa zote 59".

Sambamba na hivyo Kadogosa ameeleza mipango ya uboreshaji huduma za usafiri wa treni za bara. Kadogosa amesema TRC kupitia Serikali imeongeza behewa 22 mpya za reli ya kati (MGR) ambazo zitasaidia kuongeza safari za abiria wa mikoa ya Kigoma ,Kilimanjaro na Arusha .

**TAYARI SERIKALI IMESHATOA DOLA ZA MAREKANI MILLION**

**295.74**

***TRENI INAYOKWENDA MWENDOKASI ZAIDI YA KILOMITA 200 KWA SAA INAITWA YA MWENDOKASI, NA ZILE TRENI AMBAZO MWENDO WAKE NI CHINI YA KILOMITA 200 KWA SAA ZINAITWA TRENI ZA KAWAIDA.***



MUONEKANO WA NDANI WA TRENI YA KISASA ITAKAYOTUMIKA TANZANIA

## HATUA KWA HATUA UJENZI WA SGR

# WANANCHI

## WATOA NENO

MRADI wa ujenzi wa reli ya kisasa ya SGR ni mradi mkubwa na muhimu nchini, ni mradi ambao unafungamanishwa na ukuaji wa uchumi wa nchi.

Uwepo wake kabla na hata baada ya kukamilika una tija kubwa kwa Taifa, tija ambazo hakuna shaka yeyote zimeshaanza kuonekana kwa mtu mmoja mmoja.

Ajira lukuki za muda mrefu na mfupi zimetolewa tangu kuanza kwa mradi huo, mathalani katika kipindi cha mwaka huu wa 2023 tayari ajira 30,000 za muda mfupi zinazowahusu watu wenye fani mbalimbali zimetolewa.

Jarida hili limefanya mahojiano na baadhi ya wananchi wa sehemu ya maeneo yanakopita mradi huo na kutoa maoni yao katika masuala mbalimbali yanayohusu mradi huo muhimu hasa katika awamu ya kwanza na pili.

### 1. MUDA WA MRADI

Juma Mkomola mkazi wa Ukonga Banana, aliliambia jarida hili kuwa ingawa hana uelewa na muda uliowekwa ili kukamilisha ujenzi wa reli hiyo ya kisasa, yeye anaridhishwa na kasi ya ujenzi.

Kwa mujibu wa mpango kazi wa awali mradi wa SGR kutoka Dar es Salaam hadi Makutupora (Singida) ulipangwa kukamilika Februari 2021.

Mkataba wa kipande cha kwanza kati ya Dar es salaam na Morogoro ulisainiwa Februari 3, 2017, na ujenzi wake ulianza Mei 2, 2017 na kilitazamiwa kukamilika Novemba 2, 2019 na kipande cha Morogoro -Makutupora mkataba wake ulisainiwa Septemba 29, 2017 na ujenzi ulianza Februari 26, 2018 na kilipangwa kukamilika Februari 25, 2021.

### 2.WAKANDARASI

Bakari Mtambala mkazi wa Pugu Kajiungeni alipoulizwa juu ya ufanisi wa wakandarasi wa ujenzi wa mradi huo, yeye alisema hana mashaka nao. "Kama serikali imewaamini, kwanini mimi niwe na mashaka nao, nadhani wako vizuri tu."

Wakandarasi wa mradi huo YAPI MERKEZI ya Uturuki na MOTA- ENGIL ya Ureno waalijenga jumla ya Kilomita 722 katika vipande viwili, kipande cha Dar es Salaam-Morogoro kilomita 300 na kipande cha Morogoro -Makutupora chenye kilomita 422.

### 3. WASIMAMIZI

Akizungumzia suala la wasimamizi wa mradi huo, Mkurugenzi Mkuu wa TRC, Masanja Kadogosa alisema mhandisi Mshauri aliyesimamia mradi huu kwa niaba ya Serikali ni Kampuni ya KORAIL JV ambayo ni ubia wa Kampuni nane za KORAIL, CHEIL na DMEC kutoka Korea, MULTTECH kutoka Botswana, kampuni ya kizawa ya UNITEC kutoka Tanzania, BARAJI kutoka India, SSF kutoka Ujerumani na RINA kutoka Italia

### 4. GHARAMA

Kwa kipande cha Dar es Salaam-Morogoro Shilingi za Kitanzania Trilioni 2.7 zimetumika na kwa Kipande cha Morogoro Makutupora kiasi cha shilingi za Kitanzania Trilioni 4.4, zimetumika.

Gharama hizo zinafanya jumla ya fedha zote kwenye ujenzi huu kuwa shilingi Trilioni 7.1 ambazo ni pesa za walipa Kodi wa Tanzania.

### 5. MAPENDEKEZO

Wataalamu wa masuala ya kiuchumi walipendekeza kuwa ni vema zilipojengwa stesheni za Soga, Ruvu na Kwala, zilizopo Mkoa wa Pwani miji ipangwe kwa kupima ardhi.

Kwa eneo la Kwala ambalo litajengwa Kituo kikubwa cha mizigo na karakana za ukarabati wa matreni, mkabala na bandari kavu ilipendekezwa kuanzishwe ukanda wa viwanda (industrial Zone) ili kuvutia wawekezaji kuweka sehemu ambayo malighafi na bidhaa zao zitasafirishwa kutoka na kuingia kwenye viwanda vyao.



KUTOKA KWA

# Mhariri Mtendaji

## SGR NI CHACHU YA MAENDELEO

MRADI wa ujenzi wa reli ya kisasa maarufu kama SGR unakwenda kwa kasi na hakuna ubishi wowote mradi huo utakamilika kwa wakati na muda sahihi.

Mamilioni ya watanzania matumaini na hamu yao ni kuona mradi huo unaanza kufanya kazi ili iwawie rahisi kuutumia katika usafiri na usafirishaji.

Hakuna hata mtanzania mmoja asiyetaka kufaidi matunda ya SGR ambayo tumeambiwa ina uwezo wa kuhimili kubeba magari moshi yenye mabehewa mengi ya abiria na mizigo kwa wakati mmoja. Sisi Jarida la TZ&BEYOND tunaamini ujenzi wa mradi huu ambao ni wa kimkakati unayo tija kubwa kwa nchi na wananchi.

Ikumbukwe kuwa kwa sasa dunia imeshahamia kwenye usafiri wa reli za kisasa, hii inamaanisha hata sisi hatupaswi kujichelewesha.
Kasi ya ujenzi wa mradi huu hapa Tanzania unatusukuma kutoa pongezi za dhati kwa serikali ya Awamu ya Tano iliyokuwa chini ya Hayati Rais Dkt. John Magufuli na pia kwa serikali ya Awamu ya Sita ambayo iko chini ya Rais Samia Suluhu Hassan.

Tunaamini serikali hizi mbili pamoja na zilizotangulia zimeona umuhimu wa nchi kwenda na kasi ya mabadiliko ya dunia kwenye eneo la kiuchumi.

Kukamilika kwa ujenzi huo wa reli ya kisasa (SGR) nchini hakutainufaisha Tanzania pekee, bali hata nchi jirani zitanufaika na ujenzi wake.
Reli hii yenye upana wa mita 1.435, inatarajiwa kubeba mamilioni ya abiria na mizigo zaidi ya tani milioni 17 kwa mwaka.

Jarida la TZ&BEYOND tunaamini mradi huu mkubwa na wa muhimu utakuwa chachu na kichocheo cha maendeleo kwa watanzania wote, hivyo basi ni jukumu letu kuunga mkono, kuulinda na kuuthamini ili utuletee tija kusudiwa.

Aidha tunaiona haja ya kumpongeza Rais Samia kwa utayari wake wa kuuendeleza mradi hu una miradi mingine yote ya kimkakati.

**MUNGU IBARIKI TANZANIA, MUNGU IBARIKI AFRIKA.**



**Jimmy C. Kiango**
**MHARIRI MTENDAJI**

VISION PLUS EYE CLINIC

TIPER BULK STORAGE

TANZANIA REVENUE AUTHORITY
ISO 9001: 2008 Certified

TIB CORPORATE BANK
Your Partner Bank

KCB BANK

Air Tanzania
The Wings of Kilimanjaro

CRDB BANK
Tunakusikiliza

NSSF
BOARD OF TRUSTEES
NATIONAL SOCIAL SECURITY FUND

# SHUKRANI
za dhati kwa WASHIRIKA WETU






# Experience the power of TemboCARD

Shop locally and internationally at over 44 million merchants and 2 million ATMs

VISA

CRDB BANK

*The bank that listens*